Kristo Asiyebadilika katika Ulimwengu Unaobadilika

na

Ellis Forsman

Kristo Asiyebadilika katika Ulimwengu Unaobadilika

na

Ellis Forsman

Oktoba 7, 2011

Kristo Asiyebadilika katika Ulimwengu Unaobadilika

Waeb. 13:8

Waeb. 13:8, *"Yesu Kristo ni yeye yule, jana leo na hata milele.*

Kristo na Mwanzo

Alikuwa na Mungu toka mwanzo.

Yoh. 1:1-5, *"Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilichofanyika. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao ule uzima ulikuwa nuru ya watu. Nayo nuru yang'aa gizani, wala giza haikuiweza."*

Vitu vyote vilitengenezwa nay eye na katika yeye.

Alikuwa ni mwanga wa wanadamu wote, lakini hawakumpokea.

Yoh. 1:10-14, *"Alikuwako ulimwenguni hata kwa yeye ulimwengu ulikuwako; wala ulimwengu hauku mtambua. Alikuja kwake, wala waliowake hawakumpokea. Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndio wale waliaminilo jina lake, waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa Mungu, naye neno alifanyika mwili akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa mwana pekee atokaye kwa Baba; amejaa neema na kweli."*

Alijitoa mwenyewe kufa kwa ajili ya wanadamu wote.

Matendo. 2: 22-24, *"Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya: Yesu wa Nazareti mtu aliyedhihirishwa kwenu na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo Mungu alizifanya kwa mkono wake kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua; mtu huyu alipotelewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujuwa kwake tangu zamani, ninyi mnamsulubisha kwa mikono ya watu wabaya, mkamuua; ambaye Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti, kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao."*

Alifufuliwa katika wafu, akainuliwa, na akapewa Ufalme wa wafalme, na Bwana wa mabwana.

- Matend. 2: 36, *"Na nyumba yote ya Israeli na ijue yakini ya kwamba, Mungu amemfanya huyo Yesu mliyemsulubisha kuwa Bwana na Kristo."*
- Waef. 1:20-23, *"Aliotenda katika Kristo alipomfufua katika wafu, akamweka mkono wake wa kuume katika ulimwengu wa roho; juu sana kuliko ufalme wote, na mamlaka na nguvu, na usultani, na kila jina litajwalo, wala si ulimwenguni humu tu, bali katika ule ujao pia; akavitia vitu vyote chini ya miguu yake, akamweka awe kichwa juu ya vitu vyote kwa ajili ya kanisa, ambalo ndilo mwili wake anayekamilika kwa vyote katika vyote."*
- Wafil. 2:6-11, *"Ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho; bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa akawa anamfano wa wanadamu; tena alipoonekana ana kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam, mauti ya msalaba. Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia Jina lile lipitalo kila jina; ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu vya mbinguni, na vya duniani, na vya chini ya nchi; na kila ulimi ukiri ya kuwa YESU KRISTO NI BWANA, kwa utukufu wa Mungu Baba."*

Alipewa haki ya kushuka kutawala juu ya ufalme wa Mungu milele.

Waeb. 5:8-9, *"Na ingawa ni mwana, alijifunza kutii kwa mates ohayo yaliyompata; naye alipokwisha kukamilishwa, akawa sababu ya wokovu wa milele kwa watu wote wanaomtii."*

Ni kichwa cha kanisa katika vitu vyote kwa wakati wote kwa mamlaka yote.

Yeye habadiliki; ni yeye Yule, jana, leo na milele.

Ulimwengu unabadilika katika hatua kwa hatua, na hatimaye itachakaa kama nguo, na ipite; lakini Mfalme wetu ni wa milele. Kichwa chetu (Kristo) habadiliki na ni wa milele.

- Waeb. 1: 8-12, *"Lakini kwa habari za mwana asema, kiti chako cha enzi, Mungu ni cha milele na milele; na fimbo ya ufalme wako ni fimbo ya adili. Umepanda haki, umechukia maasi; kwa hiyo Mungu, Mungu wako amekutia mafuta, mafuta ya shangwe kupita wenzio.*

Na tena, wewe, Bwana hapo mwanzo uliitia misingi ya nchi, na mbingu ni kazi za mikono yako; hizo zitaharibika, bali wewe unadumu; nazo zote zitachakaa kama nguo, na kama mavazi utazizinga, nazo zita badilika; lakini wewe u yeye Yule, na miaka yako haitakoma."

- Waeb. 13: 8, *"Yesu Kristo ni yeye yule jana leo na hata milele."*

Kristo Anatawala kama Mfalme katika Ufalme, na Anafanyia kazi mamlaka yake juu ya kanisa lake kupitia neno lake

Mamlaka yake ya kuongea.

- Math. 17:5, *"Alipokuwa katika kusema tazama, wingu jeupe likawatia uvuli na tazama, sauti ikatoka katika lile wingu, ikasema, Huyu ni mwanangu Mpendwa wangu, ninayependezwa naye msikieni yeye."*

- 2 Petr. 1:16-18, *"Maana hatukufuata hadithi zilizotungwa kwa werevu, tulipowajulisha ninyi nguvu zake Bwana wetu Yesu Kristo na kuja kwake; bali tulikuwa tumeuona wenyewe ukuu wake. Maana alipata kwa Mungu Baba heshima na utukufu hapo alipoletewa sauti iliyotoka katika utukufu mkuu, Huyu ni mwanangu mpendwa wangu, ninaye pendezwa naye. Na sauti hiyo sisi tuliisikia ikitoka mbinguni tulipokuwa pamoja naye katika mlima ule mtakatifu."*

- Waeb. 1: 1-2, *"Mungu ambaye zamani alisema na baba zetu katika mnabii kwa sehemu nyingi na kwa njia nyingi, mwisho wa siku hizi amesema na sisi katika mwana aliyemweka kuwa mrithi wa yote, tena kwa yeye aliufanya ulimwengu."*

- Waeb. 2:1-4, *"Kwa hiyo imetupasa kuyaangalia zaidi hayo yaliyosikiwa tusije tukayakosoa. Kwa maana ikiwa lile neno lililonenwa na malaika lilikuwa imara, na kila kosa na uasi ulipata ujira wa haki, sisi je! Tutapataje kupona, tusipojali wokovu mkuu wa namna hii? Ambao kwanza ulinenwa na Bwana, kisha ukathibitika kwetu na wale waliosikia. Mungu naye akishuhudu pamoja nao kwa ishara na ajabu na nguvu za namna nyingi na kwa magawanyo ya Roho Mtakatifu, kama alivyopenda mwenyewe."*

- Yoh. 8:31-32, *"Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa*

wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli nayo hiyo kweli itawaweka huru."

Wakati wa kazi yake binafsi, Yesu anawaahidi wanafunzi wake kwamba baada ya kuondoka atawatumia Roho Mtakatifu ili awaongoze katika kweli yote:

Yoh. 14:25-26, *"Hayo ndiyo niliyowambia wakati nipokuwa nikikaa kwenu. Lakini huyo msaidizi, huyo Roho Mtakatifu, ambaye Baba atampeleka kwa jina langu, atawafundisha yote, na kuwa kumbusha yote niliyowaambia."*

Mitume waliongea jinsi Roho Mtakatifu alivyowaongoza, si kwa hekima yao au hekima ya ulimwengu.

1 Wakor. 2: 9-13, *"Maana naliandika kwa sababu hii pia, ili nipate bayana kwenu kwamba mmekuwa wenye kutii katika mambo yote. Lakini kama mkimsamehe mtu neno lolote, nami nimemsamehe; kwa maana mimi nami ikiwa nimemsamehe mtu neno lolote, nimemsamehe kwa ajili yenu mbele za Kristo, shetani asije akapata kutushinda; kwa maana hatukosi kuzijua fikira zake. Basi nilipofika Troa kwa ajili ya injili ya Kristo, nikafunguliwa mlango katika Bwana, sikuons raha nafsini mwangu kwa sababu sikumwona Tito ndugu yangu, bali niliagana nao nikaondoka kwenda Makedonia."*

Maneno yao yamekamilika na ndio mwisho.

- 2 Petr. 1:3, *"Kwa kuwa uweza wake wa Uungu umetukirimia vitu vyote vipasavyo uzima na utauwa, kwa kumjua yeye aliyetuita kwa utukufu wake na wema wake mwenyewe."*
- 2 Tim. 3: 14-17, *"Bali wewe ukae katika mambo yale uliyofundishwa na kuhakikishwa, kwa maana unajua ni akina nani uliojifunza kwao; nay a kuwa tangu utoto umeyajua maandiko matakatifu, ambayo yaweza kukuhekimisha hata upate wokovu kwa imani iliyo katika Kristo yesu. Kila andiko lenye pumzi ya Mungu, lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao, na kwa kuwaongoza, na kwa kuwaadibisha katika haki; ili mtu wa Mungu awe kamili, amekamilishwa apate kutenda kila tendo jema."*
- Wagal. 1:6-9, *"Nastaajabu kwa kuwa mnamwacha upesi hivi yeye aliyewaita katika neema ya Kristo, na kugeukia injili ya namna nyingine. Wala si nyingine, lakini wapo watu wawataabishao na kutaka kuigeuza injili ya Kristo. Lakini ijapokuwa sisi au malaika*

wa mbinguni atawahubiri injili yoyote isipokuwa hiyo tuliyowahubiri, na alaniwe. Kama tulivyotangulia kusema na sasa nasema tena, mtu awaye yote akiwahubiri ninyi injili yo yote isipokuwa hiyo mliyoipokea, na alaniwe."

- 2 Yoh. 1:9-11, *"Kila apitaye cheo wala asidumu katika mafundisho ya Kristo, yeye hana Mungu. Yeye adumuye katika mafundisho hayo, huyo ana Baba na Mwana pia. Mtu akija kwenu wala haleti mafundisho hayo, msimkaribishe nyumbani mwenu, wala msimpe salam. Maana yeye ampaye salam azishiriki kazi zake mbovu."*
- Ufun. 22: 18-19, *"Namshuhudia kila mtu ayasikiaye maneno ya unabii wa kitabua hiki, mtu yeyote akiyaongeza, Mungu atamwongezea hayo mapigo yaliyoandikwa katika kitabu hiki. Na mtu ye yote akiondoa lo lote katika maneno ya unabii wa kitabu hiki, Mungu atamwondolea sehemu yake katika ule mti wa uzima, na katika ule mji mtakatifu, ambao habari zake zimeandikwa katika kitabu hiki."*

Katika maandiko haya tunajifunza:

- Kwamba wakati wa ukristo, Mungu anaongea na wanadamu kupitia Mwanaye.
- Kwamba Mungu amethibitisha neno la Kristo na watu wake waliovuviwa kwa miujiza, maajabu, na ishara.
- Mungu atawakatalia mbali wote wanaokataa kumsikiliza mwanaye.
- Kwamba Roho Mtakatifu alipokuja kuwaongoza mitume katika kweli yote, hakusema yak wake, lakini jinsi Yesu alivyoamuru.
- Kwamba mitume waliongea kwa hekima na maneno waliopewa na Roho Mtakatifu.
- Kwamba neno la Kristo lina kila kitukinachofaa uzima na uungu.
- Kwamba Mungu anahitaji watu wakubali neno la Yesu, kama jinsi walivyo, haibadiliki, nyongeza, au kupunguzwa katika kila kitu ambacho ameongea. Neno la Kristo limekamilika, la mwisho, na limefungamana. Bila kujali kitu chochote na mabadiliko ambayo yanaweza kujitokeza katika dunia ya karne yoyote, neno la Kristo lazima likubaliwe sawa na jinsi walivyo, na wale wanao kataa kulikubali wanakatiliwa mbali.

Imani na Mawazo ya wanadamu.

Katika Ukristo kuna uwanda wa imani na uwanda wa mwazo ya wanadamu. Katika uwanda wa imani neno la Mungu ndilo la mwisho. Katika uwanda wa imani lazima kuwe na mshikamano katika neno. Anapoongea hakuna udhuru. Katika uwanda wa mawazo ya binadamu hakuna maamzi yaliyofikiwa katika kiwango cha maamzi ya wanadamu.

Wakati mwingine watu wanafikiria wengine wana vichwa vigumu wakati wanapodumu katika imani. Katika uwanda wa mawazo ya wanadamu kunaweza kukawa na ubishi kati ya mtu na mtu, lakini hatuwezi kupinga neno la Mungu.

Lazima tuangalie katika historia ya Kibiblia kuona kwamba Mungu hajawai kuhusiana na watu ambao hawaridhiki na njia zake.

- Kutoka 12:37, *"Wana wa Israeli wakasafiri kutoka Ramesesi mpaka Sukothi, walipata hesabu yao kama watu sita mia elfu watu waume waliokwenda kwa miguu bila kuhesabu watoto."*
- Kutoka 32:28, *"Na hao wana wa Lawi wakafanya kama vile alivyosema Musa, wakaanguka siku ile kama watu elfu tatu."*
- Kutoka 38:26, *"Kichwa beka maana nusu shekel, kwa kadiri ya shekel ya mahali patakatifu, kwa ajili ya kila mtu aliyepita kwa wale waliohesabiwa, aliyekuwa na umri wa miaka ishirini au zaidi, kwa ajili ya watu waume sita mia na tatu elfu, na mia tano na hamsini (603,550."*
- Hesabu 11:1-3, *"Kisha hao watu walikuwa kama wanung'unikao wakisema maovu masikioni mwa BWANA asiposikia hayo, hasira zake zikawaka; na moto wa BWANA ukawaka kati yao, ukateketeza katika mipaka ya mwisho wa marago. Ndipo watu wakamlilia Musa; naye Musa akamwomba BWANA, na ule moto ukakoma. Jina la mahali hapo likaitwa Tabera: kwa sababu huo moto wa BWANA ukawaka kati yao."*
- Hesabu 14:42-45, *"Msikwee, kwa kuwa BWANA hamo kati yenu; msipigwe na kuangushwa mbele za adui zenu. Kwa kuwa Mwamaleki na Mkanaani wako mbele yenu, nanyi mtaanguka kwa upanga, kwa sababu mmerudi nyuma msimwandame BWANA, kwa hiyo BWANA hatakuwa pamoja nanyi. Lakini walithubutu kukwea mlimani hata kileleni, ila sanduku la agano la BWANA halikutoka humo maragoni, wala Musa hakutoka. Ndipo Mwamaleki na Mkanaani waliokaa huko mlimani, wakatelemka wakawapiga na kuwaangusha, hata kufikilia Horma."*

- Katika Hesabu 16: tunaona baadhi waliinuka dhidi ya Musa: Hesabu 16:31-33,
- Hesabu 16:35, *"Kisha moto ukatoka kwa BWANA, ukawateketeza hao watu mia mbili hamsini waliofukiza uvumba."*
- Hesabu 16:41, *"Lakini siku ya pili yake mkutano wote wa wana wa Israeli wakamnung'unikia Musa, na Haruni wakasema, ninyi mmewauwa watu wa BWANA.*
- Hesabu 16:42-49, *"Basi ilikuwa hapo huo mkutano ulipokuwa umekutanika, kinyume cha Musa, na kinyume cha Haruni, wakaangalia upande wa hema ya kukutania, na tazama hilo wingu likaifunika hema, na utukufu wa BWANA ukaonekana. Na Musa na Haruni wakaenda hapo mbele ya hema ya kukutania. Naye BWANA akanena na Musa na kumwambia, Ondokeni kati ya mkutano, ili niwaangamize mara moja. Wao wakapomoka kifudifudi. Musa akamwambia Haruni, haya shika chetezo chako ukatie moto ndani yake, moto wa madhabahuni, kasha utie na uvumba juu ya moto, ukakichukue haraka, wende nacho katika huo mkutano, ukawafanyie upatanisho kwa kuwa ghadhabu zimetoka kwa BWANA; hiyo tauni imeanza. Basi Haruni akakishika chetozo kama Musa alivyonena, akapiga mbio akaenda katikati ya mkutano, na tazama tauni ilikuwa imeanza kati ya watu; akatia uvumba juu ya moto na kufanya upatanisho kwa ajili ya hao watu. Akasimama kati ya hao waliokufa na hao waliokuwa wakali hai; tauni ikazuiwa. Basi waliokufa kwa tauni walikuwa kumi na nne elfu na mia saba; zaidi ya hao waliokufa katika jambo la Kora."*
- Katika Hesabu 25: Tunapata kwamba Waisraeli waliungana wenyewe na mataifa mengine na wakaabudu Baal. Hesabu 25:9, *"Nao waliokufa kwa hilo pigo walikuwa watu elfu ishirini na nne hasabu yao."*
- Hesabu 20:10-11, *"Musa na Haruni wakawakusanya kusanyiko mbele mwamba, akawaambia, sikiwni, sasa enyi waasi; je! Tuwatokezee maji katika mwamba huu? Musa akainua mkono wake akaupiga ule mwamba kwa fimbo yake mara mbili, maji yakatoka mengi, mkutano wakanywa na wanyama wao pia."*

Musa alitenda dhambi kwa kuchukua baadhi ya sifa yeye binfsi kwa kutumia neno *"sisi"* badala ya kumpa Mungu sifa zote.

- Hesabu 20: 12, *"BWANA akamwambia Musa na Haruni, kwa kuwa hamkuniamini mimi ili kunistahi mbele ya macho ya wana wa*

Israeli, basi kwa sababu hiyo, hamtawaingiza kusanyiko hili katika ile nchi niliyowapa."

- Kumbu. 34:4, *"BWANA akwambia, hii ndiyo nchi niliyowaapia Ibrahimu na Isaka, na Yakobo, nikisema nitawapa wazao wako. Basi nimekuonyesha kwa macho yako, lakini hutavuka huko."*
- Hesabu 14:30, *"Hakika yangu hamtaingia ninyi katika nchi, ambayo niliinua mkono wangu ya kwamba nitawaketisha humo, isipokuwa Kalebu mwana wa Yefune, na Yoshua mwana wa Nuni."*

Tukiangalia ni wangapi wana wa Israeli waliokufa kwa sababu ya dhambi zao, tunawezaje kutarajia kukwepa Siku ya Hukumu kwa sababu ya dhambi zetu? Yesu Kristo ni yule, jana leo, na milele.

Waeb. 13:8-9, *"Yesu Kristo ni yeye yule, jana, leo, na milele."* Usibebwe na upotofu pamoja na injili ya kigeni.